JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

# SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA

ISO 9001:2015 Certified

*Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali*

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU PICHA MJONGEO (VIDEO) ZINAZOSAMBAA KWENYE MITANDAO YA KIJAMII KUHUSU BIDHAA ZA VILAINISHI (ENGINE OIL)

**Dar es Salaam, 2026-02-13**

Hivi karibuni, kumekuwa na taarifa za picha mjongeo (video) zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii zikionesha baadhi ya watu wasio waaminifu wakifungasha bidhaa za vilainishi vya injini (engine oil) katika maeneo yasiyo rasmi, huku wakitumia chapa (brand) za baadhi ya kampuni kinyume na taratibu. Aidha, picha mjongeo nyingine inaonesha namna ya kufuta na kubadili tarehe ya muda wa matumizi wa bidhaa (shelf life) kwenye kifungashio cha aina ya kopo.

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linapenda kuujulisha umma kuwa, maudhui ya vitendo hivyo ni kinyume cha Sheria ya Viwango Sura 130 na Shirika linatoa rai kwa wale wote wanaosambaza taarifa hizo kuacha mara moja. TBS inaendelea kufuatilia kwa ukaribu suala hilo kwa kushirikiana na vyombo vingine vya udhibiti na usalama ili kuzuia usambazaji na uuzaji wa bidhaa hafifu zinazoonekana na kuwafikisha watuhumiwa katika vyombo vya sheria.

Shirika kupitia mifumo yake ya udhibiti litaendelea kushirikiana kwa karibu na wadau wa sekta husika ili kuhakikisha bidhaa za vilainishi zinaendelea kukidhi matakwa ya viwango husika, ili kuhakikisha mteja anauziwa bidhaa iliyo sahihi.

Aidha, Shirika linatoa wito kwa umma kutoa taarifa kupitia kituo cha huduma kwa wateja kwa namba **0800110827,** ofisi ya TBS iliyo karibu nao au ofisi ya halmashauri pindi wanapobaini maeneo/matendo yasiyo rasmi yanayojihusisha na uzalishaji au uuzaji wa bidhaa hizo.

Imetolewa na:

Gladness H Kaseka
**MENEJA WA UHUSIANO NA MASOKO**

**TBS MAKAO MAKUU**
Shirika la Viwango Tanzania
Barabara ya Sam Nujoma / Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
Simu Na: +255 22 245 0298/ +255 22 245 0206
Nukushi: +255 22 2450959
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
Barua pepe: info@tbs.go.tz
Tovuti: http://www.tbs.go.tz
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya wateja: malalamiko@tbs.go.tz
Twitter: TBS_Tanzania
Instagram: tbs_Viwango

**TBS KANDA YA KATI**
Jengo la Kambarage
S. L. P. 2956
DODOMA, TANZANIA
Simu Na:
+255 26 2520310

**TBS KANDA YA ZIWA**
Jengo la NSSF, Ghorofa ya 3
S. L. P. 1814
MWANZA, TANZANIA
Simu Na:
+255 28 2505044

**TBS KANDA YA KASKAZINI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 2399
ARUSHA, TANZANIA
Simu Na:
+255 27 2520143

**TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7
S. L. P. 1674
MBEYA, TANZANIA
Simu Na:
+255 25 2502848

**TBS KANDA YA KUSINI**
Jengo la MTUWASA
S. L. P. 1396
MTWARA, TANZANIA
Simu Na:
+255 23 2334477

**TBS KANDA YA MAGHARIBI**
Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2
S. L. P. 1276
KIGOMA, TANZANIA
Simu Na:
+255 28 2804023